JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WILAYA YA MAFIA

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

112 Mafia, Pwani Tanzania
Simu ; +255 (0)232 010205,
Tovuti ; www.ruwasa.go.tz,
Baruapepe; mafiadm@ruwasa.go.tz

RUWASA

MKATABA WA AJIRA YA UBEBAJI/USAFIRISHAJI WA BOMBA KUTOKA OFISI YA RUWASA HADI VIJIJI VYA MRADI WA UPANUZI WA SKIMU YA MAJI MLONGO-MIBURANI NA SKIMU YA MAJI KIRONGWE-JOJO

MKATABA HUU unafanyika leo tarehe 15 mwezi 02 2022

BAINA YA

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA (RUWASA), WILAYA YA MAFIA S. L. P 112 (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "**Mwajiri au RUWASA**") Kwa upande mmoja;

NA

NDG. KISIWA FARMING LTD, **wa S. L. P.** 63 **MAFIA**: (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **mwajiriwa au "Msafirishaji"**) kwa upande mwingine.

KWAMBA Kwa Pamoja Mwajiri na Mwajiriwa watajulikana kama pande mbili za Mkataba.

AMBAPO;

a) Mwajiri ni Wakala wa serikali wenye jukumu la kutekeleza ujenzi wa Miradi ya Maji vijijini na kusimamia utoaji wa huduma ya Maji na usafi wa mazingira vijijini na yenye makao makuu yake jijini Dodoma.

b) Mwajiriwa ni Msafirishaji anayefanya shughuli za usafirishaji katika eneo la Mafia.

c) Mwajiriwa anakubali matakwa ya mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kufanya kazi ya usafirishaji wa vifaa vya ujenzi katika mradi wa Upanuzi wa skimu ya maji Mlongo hadi kijiji cha Miburani.

MKATABA HUU UNASHUHUDIA Kwa pande zote mbili kukubaliana kama ifuatavyo;

1. MADHUMUNI YA MKATABA

Mkataba huu ni kwa ajili ya Usafirishaji wa vifaa vya ujenzi eneo la kijiji cha miburani ambapo Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zifuatazo;

- Kukodi trekta kusafirisha bomba kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa mtandao wa usambazaji wa maji skimu ya maji kijiji cha Mlongo-Miburani na Kirongwe-Jojo kwa siku 10.

CamScanner

- Kwa siku 11 @ 250,000/- sawa na Tshs. 2,750,000/-
- Kukodisha "concrete mixer m/c" kwa siku tano (5).
  - Kwa siku 5 @ 200,000/- sawa na Tshs. 1,000,000/-
- Kukodisha "porker m/c" kwa siku tano (5).
  - Kwa siku 5 @50,000/- sawa na Tshs. 250,000/-

2. MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI

Kazi ya Usafirishaji bomba itafanywa kwa muda wa SIKU KUMI (10), kadri ya kasi ilivyohitajika kwa fundi ujenzi kukamilisha kazi.

3. MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI

Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha Tshs. 4,000,000/- **(Milioni Nne Tu)** Kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zilizoainishwa hapo juu.

a) Malipo ya mwajiriwa yatakuwa ni kwa fedha za Kitanzania tu (Tanzanian Shillings).

b) Malipo hayo yatalipwa katika Akaunti ya Mwajiriwa, Na. 2151001056 1-)

c) Malipo ya mwajiriwa yatalipwa kulingana na kazi baada ya ukaguzi na kukubalika na mwajiri ndani ya muda uliokubalika kwa mujibu wa Sheria ya manunuzi ya mwaka 2003, kadri ya maafikiano na Mwajiri.

4. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri ambaye atawakilishwa na msimamizi wa kazi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa na msafirishaji;

b) Kuwasiliana na uongozi wa eneo husika namna ya kuwashirikisha wananchi/Chombo Cha Watumia Maji Ngazi ya Jamii itakapo hitajika.

c) Endapo kazi itakayofanywa na mwajiriwa haitafikia viwango vya ubora unaotakiwa,Mwajiri atachukua hatua stahiki dhidi ya Mwajiriwa huyo;

d) Kuhakikisha kuwa endapo Mwajiriwa atafanya kazi isiyokidhi viwango au isiyoridhisha, Mwajiriwa huyo anarekebisha au kurudiwa upya kazi hiyo kwa gharama zake.

Mwajiri ambaye atawakilishwa na Msimamizi wa kazi, atakuwa na haki kama ifuatavyo:

e) Kupata kazi iliyo bora kutoka kwa mwajiriwa.

5. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRIWA

Mwajiriwa ambaye ni Msafirishaji atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kuhakikisha kuwa anatekeleza usafirishaji wa vifaa kama ilivyoelekezwa kwenye sehemu ya 1(Madhumuni ya mkataba);

b) Kuhakikisha kuwa anawajibika kufanya kila jambo ambalo kwa ujumla wake litaleta mafanikio na kuepuka uharibifu wa mali kwenye kazi ya usafirishaji;

c) Atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, uadilifu, umakini na weledi mkubwa na endapo atatekeleza kinyume na matakwa haya hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake;

d) Atawajibika kwa Msimamizi wa Mradi *(Project Manager)* kwa utendaji wa kazi.

e) Kuhakikisha malipo ya wasaidizi wake yanafanyika kwa wakati; na

CamScanner

Mwajiriwa atakuwa na haki kama ifuatavyo:

f) Kupata malipo kutokana na kazi aliyotekeleza na kukubaliana na mwajiri kadri ya mkataba.

6. UTOAJI WA MIKATABA MIDOGO

Mwajiriwa anaweza kuingia Mikataba midogo kiasi kadhaa ya utekelezaji wa kazi na vibarua (Casual Labourers) watakaokuwa chini ya usimamizi wake.

7. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na Sheria za Tanzania.

8. USULUHISHI WA MIGOGORO

Endapo kutatokea mgogoro wa aina yeyote baina ya mwajiri na mwajiriwa wa kuhusu utekelezaji wa mradi huu:

a) Pande zote mbili zita tatua mgogoro huo kwa njia ya amani ya mazungumzo ambapo makubaliano ya pande hizi mbili yatapelekea mkataba huu kufanyiwa mrekebisho; na

b) Endapo mgogoro huo utashindikana kutatuliwa kwa njia ya amani ya mazungumzo pande zote mbili zinaweza kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

9. KUSITISHA MKATABA

Mkataba huu unaweza kusitishwa endapo upande mmoja au pande zote mbili za Mkataba zitashindwa kutekeleza wajibu wake au masharti ya Mkataba huu.

KWA USHUHUDA HUU, Pande zote mbili zinawekwa Saini zao katika Mkataba huu siku na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

KWA NIABA YA MWAJIRI (RUWASA)

Jina: ENG. CLEMENT K. LYOTO

Saini: [signature]

Cheo: Meneja wa RUWASA (W).
(Project Manager)

Tarehe: 15/02/2022

MENEJA WA RUWASA
MAFIA

Shahidi:

Jina: SOPHIA MSHANA

Saini: [signature]

Cheo: ENGINEER

Tarehe: 15-02-2022

KWA NIABA YA MWAJIRIWA (MSAFIRISHAJI)

Jina: SAMWEL J. BONGI

Saini: [signature]

Cheo: GENERAL MANAGER.

Tarehe: 15/02/2022

Shahidi:

Jina: MARK KIHULA.

Saini: M.K.

Cheo: GENERAL MANAGER

Tarehe: 15/02/2022

CamScanner